

11-Makhaarij Al-Huruwf (Matokeo Ya Herufi)

مَخْرَجِ الحُرُوفِ Makhaarij Al-Huruwf - Matokeo ya herufi: Katika Kiarabu, ni wingi wa neno “makhraj” ambako katika istiliahi ya Tajwiyd ni sehemu inayotokea sauti ya kila herufi na kutofautiana na herufi nyinginezo, iwe kwa njia ya uhakika au kwa njia ya kukadiria.

Vipi Kuzitambua Herufi Katika Kuzitamka

Kutambua matokeo ya herufi husika na vipi inatamkwa, inapasa kuitia kila herufi sukuwn na kuweka hamza kabla yake, mfano: أَبْ أَتْ أَثْ أَجْ أَخْ: أُنْna pale itakapo malizia sauti ndio huwa makhraj yake.

Kwa ujumla herufi zote zinatoka katika maeneo matano makuu ambayo ndani yake hupatikana makhaarij kumi na saba madogo madogo kwa uchambuzi:

1	الجَوْف	Al-Jawf	Uwazi wa kinywa na koo
2	الحَلْق	Al-Halq	Koo
3	اللِّسَان	Al-Lisaan	Ulimi
4	الشَّفَتَان	Ash-Shafataan	Midomo miwili
5	الْحَيْشُوم	Al-Khayshuwm	Puani

Maeneo makuu ya kutokea herufi

